# Hazina ya Covid-19 ya Kaunti ya Columbus-Franklin ya Kuinua na Kurejesha Biashara Ndogondogo

Hazina ya Covid-19 ya Kaunti ya Columbus-Franklin ya Kuinua na Kurejesha Biashara Ndogondogo hupeana ruzuku na mikopo yenye riba za chini kwa biashara Ndogondogo zilizoathirika na janga la COVID -19.

### Mpango huu unanuia kupeana ufadhili kwa biashara Ndogondogo ili kuzisaidia:

- Kustahimili janga, kudumisha huduma na waajiriwa;
- Kuwapa mafunzo upya waajiriwa;
- Kurejea biasharani salama ili kuwahudumia wateja; na
- Kufaidi kutokana na fursa za ukuaji

## Hazina hii iko na aina tatu za misaada:

- **Msaada wa Kifedha-** kupeana msaada wa kifedha kwa biashara Ndogondogo zilizopo zikiwemo zile za Mapato ya Chini na ya Kati (MLI) Katika eneo la Jiji la Columbus lakini katika mizani ya Kaunti ya Franklin, na wanabiashara wote kwenye MCK wamehitimu.
- **Msaada wa Uagizaji wa Vifaa Binafsi Vya Kujikinga ( PPE) –** kupeana msaada wa kifedha kusaidia biashara ndogo ili kupata Vifaa Vya Kujikinga PPEs na/ama kuunda hali zinazofaa za kiafya/kiusalama ili kukabili janga la COVID -19 na kuwasaidia kufungua tena biashara zao katika Jiji la Columbus . Hitaji hili pia ni kwa biashara zilizo nje ya Jiji la Columbus lakini katika mizani ya Kaunti ya Franklin.
- **Msaada wa Mafunzo na Utendakazi-** kupeana msaada wa mafunzo na utendakazi kabla na baada ya kujiandikisha kwa walioomba ruzuku/ mkopo na wanaoupata, wenye biashara ndogo zilizopo, kwa nia ya kudumisha huduma na pia kudumisha wafanyikazi waliopo na hata kuongeza wengine katika Jiji la Columbus na kufuatilia viwango vya miradi yao.

## Jinsi ya kujisajili

- Usajili utafunguliwa Juni 9, 2020 saa kumi na moja jioni ET. Maombi yatakubalika kwa awamu hadi jioni ya Julai, 17,2020 au hadi ufadhili utakapokwisha.
- Wanabiashara wataunganishwa na Mashirika Ya Kieneo Ya Kusaidia Mwanabiashara (ESOs). Tuma maombi hapa.
- Jifunze mengi kwa: https://bit.ly/CBUSRecoveryFund

## Mashirika ya Msaada wa Wajasiriamali na Watoaji wa Msaada wa Ufundi

## Washirika wa Ufadhili na Utetezi

## Wabia Jirani wa Rufaa

## Jinsi Maombi Yanavyotathminiwa

- Wabia katika Mashirika ya Kusaidia Wanabiashara watahakikisha maombi yote yamejazwa kwa ushirikiano na mwenye biashara
- Kamati angalizi itapitia yale maombi na kuzipa kipaumbele biashara ambazo:
- Zinadhihirisha uwezekano mkubwa wa kuwepo baada ya COVID- 19
- Ziko kwenye harakati ya kufanya mauzo na kudumisha wafanyikazi
- Zimeonyesha bajeti zao vile watatumia fedha hizo

## Programu ya Ufadhili na Yanayohitajika

| | Ruzuku za Kujinusuru | Ruzuku za biashara ndogo kujinusuru salama Vifaa Vya Kujikinga (PPE) | Mikopo ya Pivot |
|---|---|---|---|
| **Kusudi** | • Kutoa msaada wa kifedha kwa biashara ndogo, katika maeneo ya mapato ya chini na kati kwenye Jiji au kwa wanabiashara wa LMI walio nje ya Jiji lakini kwenye Kaunti ya Franklin<br>• Ruzuku ya kusaidia kudumisha upeanaji wa huduma zao hadi mwisho wa janga la COVID-19<br>• Lengo la kudumisha huduma za biashara zilizopo na kudumisha kazi | • Kupeana msaada wa kifedha kwa biashara ndogo Jijini na Kaunti ya Franklin ili zipate PPE<br>• Pia husaidia kuimarisha hali za kiafya/ kiusalama kuzuia COVID 19 ili wakazi wa Jiji na wafanyikazi wawe salama | • Kupeana mikopo yenye riba ya chini kwa wenye biashara ndogo na wa LMI walio Jijini na eneo la Kaunti ya Franklin nje ya Jiji ikiwa biashara imepata wanunuzi wapya kwa bidhaa mpya au zilizoko au huduma mpya au laini za bidhaa ambazo biashara inawezapanukia<br>• Mikopo kwa biashara za mjini Inawezafutiliwa mbali baada ya miezi 3 zikiafikia mahitaji ya muhimu ( ikiwemo kujihusisha na mpango wa Msaada wa Kiufundi na kutumia fedha vyema) |
| **Nani Anahi timu?** | • Biashara kwenye maeneo ya LMI (ona ramani) katika mipaka ya manispaa ya Jiji la Columbus au wanabiashara za LMI nje ya jiji lakini katika Kaunti ya Franklin.<br>• Chini ya wafanyikazi 25, kipaumbele kitapeanwa kwa wafanyikazi chini ya 5<br>• Mauzo yaliyopungua (>25%) kwa sababu ya COVID- 19 tangu Machi 17 , 2020 | • Biashara kwenye maeneo ya mipaka ya manispaa ya Jiji la Columbu au katika Kaunti ya Franklin.<br>• Wafanyikazi <25 | • Biashara kwenye maeneo ya LMI katika mipaka ya manispaa ya Jiji la Columbus<br>• Chini ya wafanyikazi 25, kipaumbele kitapeanwa kwa wafanyikazi chini ya 5<br>Ikiwa biashara yako iko nje ya Jiji la Columbus lakini katika mizani ya Kaunti ya Franklin, na ungehitaji mkopo unaweza kuwasiliana moja kwa moja na Taasisi ya Uchumi na Maendeleo ya Jamii kwa https://www.ecdi.org/invest/loan-program |
| **Ufadhili kwa Kila Biashara** | • Ruzuku za hadi $10,000<br>• Kiwango kitaamuliwa baada ya maombi kupitiwa | • Ruzuku hadi $5,000 kurejeshwa kutokana na ununuzi wa PPE na maagizo ya kiafya /kiusalama kutokana na COVID-19 tangu 3/17/20, na hitaji la uwaiano wa 1:1 kwa biashara itakayofuzu<br>• Kiwango kitaamuliwa baada ya maombi kupitiwa | • Mkopo usiozidi 50% ya Biashara/Upanuzi wa Mradi/Gharama ya Uchaguzi hadi $20,000(iliyo ya chini)<br>• Riba ya chini, kiwango cha 1%<br>• Kiwango kitaamuliwa baada ya maombi kupitiwa |
| **Nini kinachohitaj ika?** | • Cheti kilichotiwa sahihi cha biashara kuonyesha ulipaji ushuru<br>• Cheti binafsi cha ulipaji ushuru kilichotiwa sahihi<br>*Fomu ya usajili iliyojazwa ikijumuisha:*<br>• Maelezo ya kimsingi ya biashara<br>• Maelezo ya athari za COVID-19 kwa biashara (ikijumulisha mapato)<br>• Mpango unaopendekezwa wa kujinusuru baada ya COVID-19<br>• Bajeti ya matumizi ya fedha<br>• Dhibitisho ikiwa biashara imepokea ufadhili wa PPP ama EIDL<br>*Ikifadhiliwa:*<br>Biashara lazima ishiriki katika programu ya Msaada wa Kiufundi ya lazima<br>• Biashara lazima ipeane ripoti za jinsi ilivyo kila mwaka | • Risiti za 3/17/20 au baadaye za PPE na ununuzi wa vifaa vya Usalama/Afya vya COVID-19 kama thibitisho ya malipo ya biashara<br>• Thibitisho kama biashara imepokea ufadhili wa PPP au EIDL<br>*Ikifadhiliwa:*<br>• Biashara lazima ipeane ripoti za jinsi ilivyo kila mwaka | • Cheti kilichotiwa sahihi cha biashara kuonyesha ulipaji ushuru<br>• Cheti binafsi cha ulipaji ushuru kilichotiwa sahihi<br>• *Fomu ya usajili iliyojazwa ikijumuisha:*<br>• Maelezo ya kimsingi ya biashara<br>• Maelezo ya athari za COVID-19 kwa biashara (ikijumulisha mapato)<br>• Mpango unaopendekezwa wa kujinusuru baada ya COVID-19<br>• Bajeti ya matumizi ya fedha<br>• Dhibitisho ikiwa biashara imepokea ufadhili wa PPP ama EIDL<br>• *Ikifadhiliwa:*<br>Biashara lazima ishiriki katika programu ya Msaada wa Kiufundi ya lazima<br>• Biashara lazima ipeane ripoti za jinsi ilivyo kila mwaka |

## Kamati ya Mapitio

## Maswali ya Jumla ya Mpango huu

***Ninawezaje Kutuma maombi?***

Wamili wa biashara wataunganishwa na Mashirika Ya Kieneo Ya Kusaidia Mwanabiashara (ESOs). Tuma maombi hapa.

***Ufahili wa kwanza wa programu hii ni wa kiasi gani?***

Ufahili wa jumla wa programu hii ni $7.75M, ukigawanywa kwa huduma tatu-Ruzuku za Kujinusuru, Ruzuku za Kunusuru biashara Ndogondogo (PPE), Mikopo ya Pivot

***Je, biashara zinaweza kutuma maombi kwa programu nyingi?***

Ndio.

***Biashara za kila aina zinahitimu?***

La. Biashara za kamari na vileo, biashara za utumbuizaji wa watu wazima, au biashara zingine za aina hii hazihitimu kwa programu hii. Ikiwa ungependa kutuma maombi na huna hakika ikiwa biashara yako inahitimu, tafadhali uliza katika tovuti hapa.

***Nani wa kuulizwa kwanza maswali ya programu?***

Tovuti ya Hazina ya COVID-19 ya Columbus-kaunti ya Franklin wa Kuinua na Kunusuru Biashara Ndogondogo (yapatikana hapa) ndiyo haswa ya kuulizwa maswali yanayohusiana na programu. Iwapo wamiliki wangependa kutuma maombi, wawasilishe fomu ya ombi la Kufanyiwa Ulinganisho kwa tovuti ili waunganishwe na mshirika ya ESO ili kutuma maombi. Mbia wa ESO anaweza kusaidia kujibu maswali kuhusu uhitimu na utumaji maombi.

***Nilipata ufadhili kutoka programu za serikali za kukabili COVID-19 (PPP au EIDL) lakini hazitoshelezi biashara yangu. Je, naweza kuomba ufadhili kwa mojawapo ya programu hizi?***

Ndio-programu hizi zinapatikana kwa wanabiashara waliopokea msaada wa serikali *

*Ikiwa biashara yako iko nje ya Jiji la Columbus lakini katika mizani ya Kaunti ya Franklin, hauhitimu ikiwa ulipokea msaada wa serikali wa programu ya PPP au EIDL.

***Je, kuna nyenzo zilizochapishwa za biashara vinavyoeleza kuhusu ufadhili huu?***

Ndio, unaweza kupakua nakala ya PDF kwenye tovuti ya Hazina ya COVID-19 ya Columbus- kaunti ya Franklin wa Kuinua na Kunusuru Biashara Ndogondogo (iko hapa.

***Tovuti ya Hazina itafanyakazi katika simu?***

Ndio. Tovuti ya Hazina ya COVID-19 ya Columbus-Kaunti ya Franklin ya Kuinua na Kunusuru Biashara Ndogondogo (inapatikana hapa), imeundwa ifanyekazi katika simu ya rununu.

***Inachukua muda gani biashara kufadhiliwa ikishapokezwa kwa mbia wa ESO?***

Tukitarajia riba ya juu programu ikifunguliwa, tunalenga kupeana fedha za kwanza kufikia Juni 30. Baada ya tarehe hii, tunalenga kutoa fedha kwa kila wiki mbili, awamu ya mwisho ikiwa wiki mbili baada ya mwisho wa muda wa programu.

***Ikiwa biashara haihitimu kupewa ruzuku, je, kuna nyenzo zingine au maelekezo ya kuisaidia?***

Nia yetu ni kusaidia biashara katika kipindi hiki kigumu. Ikiwa biashara haijafadhiliwa kupitia hii programu, inafaa idumishe uhusiano na shirika la ESO, ambalo litapeana ushauri wa utendakazi kwa maswala ya biashara. Pia kuna mwelekezo wa biashara ndogo pamoja na rasilimali kwa biashara katika tovuti ya Columbus-Kaunti ya Franklin ya COVID-19 wa Kuinua na Kunusuru Biashara Ndogondogo(inapatikana hapa)

***Je kutakuwa na ramani ya kuonyesha wilaya za LMI katika tovuti ili kuamua wanaohitimu?***

Idara ya Teknolojia ya Jiji la Columbus imeunda ramani ya kuonyesha sehemu zilizohitimu katika jiji. Hiki kifaa kitakuruhusu kuweka anwani au kuangazia sehemu mahalumu ya kijografia kwenye ramani kuthibitisha ikiwa –a:) iko jijini Columbus na –b:)eneo linalohitimu LMI. Pata ramani hapa.

***Kutokana na kuharibiwa kwa biashara na ghasia za kitaifa za hivi karibuni, je ruzuku/mkopo huu utapanuliwa?***

Sio kwa wakati huu. Biashara zinazotuma maombi zapaswa kuwa zikitafuta msaada haswa kwa kujinusuru kutokana na COVID-19 na kulingana na masharti ya LMI yaliyolengwa na programu hii.

***Je, wenye biashara walio na rekodi ya uhalifu mkubwa wanajumuishwa?***

Ndio.

***Je biashara zilizo na madeni (ushuru, faini na/au malipo) ya jiji la Columbus zinahitimu?***

La-programu hii itafadhili biashara zisizo na madeni kwa jiji la Columbus.

***Je na ikiwa biashara ina mpango wa kulipa ushuru unaodaiwa?***

Ndio, hizo biashara zinahitimu, mradi tu ziko katika hali ya kuendelea kulipa. Thibitisho la hali ya sasa ya malipo litaandamanishwa na maombi. Biashara pia zafaa kuwa zimelipa madeni yote ya Kaunti ya Franklin.

***Je ni madeni tu ya Columbus yatakayofanya biashara kuondolewa, au zitaondolewa kutokana na madeni ya Kaunti ya Franklin au Jimbo la Ohio pia? (k.m., ushuru wa mali, madeni ya biashara za kitaifa)***

Deni ambalo halijalipwa kwa Columbus ndicho kiini cha kuondolewa. Jiji halitaangalia madeni kwa Kaunti, Jimbo, au Serikali kuu. Kama tulivyosema awali Biashara pia zafaa kuwa zimelipa madeni yote ya Kaunti ya Franklin.

***Je ukiukaji wa sheria za biashara utaondoa biashara isihitimu?***

Ndio. Biashara ambazo zimekiuka sheria hazitahitimu. Jiji litawajibika kupeana orodha ya sasa ya ukiukaji. Pia biashara zilizopeanwa kwa ofisi ya ya sheria ya jiji kwa kutozingatia sheria za kiafya kwa umma za COVID-19 hazitahitimu.

***Je walio na biashara binafsi wanahitimu?***

Ndio.

***Je biashara zisizo za kifaida zinaweza kutuma maombi?***

La, programu zetu zinanuia kusaidia biashara za faida pekee.

***Je na biashara za faida zilizomilikiwa na shirika lisilo la kifaida zinaweza kujisajili?***

Biashara za faida zilizomilikiwa na shirika lisilo la kifaida zinahitimu, mradi tu zinatimiza masharti mengine yote. Maombi lazima yatumwe kupitia biashara ya kifaida, wala sio kampuni isiyo ya kifaida.

***Ni vipi na lini nitatuma maombi?***

Hazina ya COVID-19 ya Columbus-Kaunti ya Franklin ya Kuinua na Kunusuru Biashara Ndogondogo utafunguliwa Juni 9, 2020 5p.m. EST. Maombi yatakubaliwa kwa awamu hadi Julai 17, 2020 5p.m. EST.

## Maswali ya Hitimu na Masharti

## *Programu ya Ruzuku ya Uinuaji wa Biashara Ndogo*

***Je biashara yangu inahitimu?***

Ili kuhitimu, biashara inapaswa:

- Iwe katika maeneo ya kipato cha chini au kati kwenye Jiji la Columbus. (kiungo cha kuthibitisha ikiwa biashara iko katika eneo linalohitimu itapeanwa kwenye tovuti)*
- Iwe ya kifaida
- Isiwe na madeni (ushuru, faini na/au malipo) ya Jiji la Columbus au Kaunti ya Franklin.
- Iwe na wafanyikazi wasiozidi 25 katika maeneo yote
- Ithibitishe kwamba imepoteza angalau asilimia 25 ya mapato katika eneo iliyopo tangu amri ya "Kaa Nyumbani" ilipoanza kutekelezwa mnamo Machi 17

***Ninawezaje kutumia ufadhili huu?***

Ruzuku hii inaweza kutumika kulipa wafanyikazi, gharama za biashara, malipo ya kukodi au ku-lisi na ununuzi wa vitabu muhimu vya biashara. Fedha haziwezi kutumika kuboresha mtaji au matumizi ya kibinafsi

***Je harakati ya kupitisha maombi ya ruzuku inahusisha kuangalia ikiwa una fedha au sharti la hakikisho binafsi?***

La.

***Je nitathibitishaje kwamba nimepoteza angalau asilimia 25 ya mapato tangu amri ya Kaa-Nyumbani ilipoanza kutekelezwa?***

Hii itaonyeshwa kwa malinganisho ya mapato ya mwaka-kwa-mwaka au mwezi-kwa-mwezi wa mapato Aprili 2020.

***Ni stakabadhi gani ninahitaji kuandamanisha na maombi?***

- Cheti cha hivi punde cha ulipaji ushuru wa biashara
- Cheti cha hivi punde cha ulipaji ushuru wa binafsi.

*Ikiwa biashara yako iko nje ya Jiji la Columbus, lakini katika mizani ya Kaunti ya Franklin, biashara inahitimu ikiwa mmiliki anahitimu kama LMI.

## *Ruzuku za Biashara Ndogo Kujinusuru Salama (PPE)*

***Je biashara yangu inahitimu?***

Ili kuhitimu, biashara inapaswa:

- Kuwa kwenye Jiji la Columbus au nje ya Jiji la Columbus lakini katika mizani ya Kaunti ya Franklin
- Iwe ya kifaida
- Isiwe na madeni (ushuru, faini na/au malipo) ya Jiji la Columbus au Kaunti ya Franklin.
- Iwe na wafanyikazi wasiozidi 25 maeneo yote

***Ninawezaje kutumia ufadhili huu?***

Ruzuku hii lazima itumike kununua vifaa vya kujikinga kibinafsi na/au kuboresha hali za afya/usalama vinavyofaa vya COVID-19 vinavyohitajika kufungua tena biashara zao salama. Matumizi yanayokubalika ni usambazaji wa PPE kwa wafanyikazi na wateja (k.v. barakoa/ngao, glovu, viyeyuzi ) pamoja na mabadiliko yoyote kwenye sehemu ya kazi ili kukubaliana na masharti ya kiafya na kiusalama kuzuia COVID-19(k.v. kinga za kunyunyuzia, kinga za kupiga chafya, COVID-19 prevention signage, na mabango ya kuweka umbali). Hii inaweza kujumulisha gharama za wafanyikazi, mradi tu biashara zitadhihirisha kwamba wafanyikazi zaidi walihitajika kushughulikia nafasi iliyopanuliwa kukubaliana na masharti ya umbali (k.v., upanuzi wa maegesho).

***Je matumizi ya kazi yanakubaliwa kwenye Programu ya Kurejea Salama?***

Kama ilivyoelezwa hapo juu pekee.

***Je ruzuku ya PPE ni ya Kurejesha fedha zilizonunua vifaa au biashara inaweza kutumia hii ruzuku kununua PPE mpya?***

Ni ruzuku ya Kurejesha, basi itahitajika kuwe na thibitisho la ununuzi (k.v. risiti au ankara). Ruzuku inaweza kupeanwa kwa ununuzi uliotekelezwa na/au ununuzi ujao (mradi tu thibitisho la ununuzi na gharama inapeanwa).

***Je harakati ya kupitisha maombi ya ruzuku inahusisha kuangalia ikiwa una fedha au sharti la hakikisho binafsi?***

La.

***Ni stakabadhi gani ninafaa kuandamanisha na maombi?***

Tafadhali wasilisha risiti na/au ankara za uagizaji zilizotumika kuagiza PPE za wafanyikazi ili kusaidia kuanza biashara tena kwa salama, au ikiwa kuna gharama za kazi zilizoongezeka, rekodi za malipo kwa kipindi husika na stakabadhi ya vile kazi hii ilisaidia kukubaliana.

## Mikopo ya Pivot

***Je biashara yangu inahitimu?***

Ili kuhitimu, biashara inapaswa:

- Iwe katika maeneo ya kipato cha chini au kati kwenye Jiji la Columbus. (kiungo cha kuthibitisha ikiwa biashara iko katika eneo linalohitimu itapeanwa kwenye tovuti)*
- Iwe ya kifaida
- Isiwe na madeni (ushuru, faini na/au malipo) ya Jiji la Columbus au Kaunti ya Franklin.
- Iwe na wafanyikazi wasiozidi 25 maeneo yote
- Ithibitishe kwamba imepoteza angalau asilimia 25 ya mapato katika eneo iliyopo tangu amri ya "Kaa Nyumbani" ilipoanza kutekelezwa

*Tambua kwamba: Ikiwa biashara yako iko nje ya Jiji la Columbus lakini katika mizani ya Kaunti ya Franklin na biashara inatafuta ufadhili tafadhali tazama hitimu na maswali kwa: https://www.ecdi.org/small-business-loans/

***Je, nawezaje kutumia ufadhili huu?***

Mikopo hii imenuiwa kusaidia biashara kuinua modeli za biashara zao ikizingatiwa changamoto zilizosababishwa na COVID-19. Matumizi yanayokubalika hujumlisha soko mpya kwa bidhaa zilizopo ama huduma mpya au laini za bidhaa ambazo biashara zinaweza kupanuka kwa nia ya kudumisha shughuli za biashara zilizopo, huku zikidumisha kazi zilizopo, kuunda nafasi mpya za kazi kuwekeza kwa mtaji kwa sababu ya ukuaji wa soko usiotarajiwa.

***Mikopo hii inasameheka?***

Mikopo itastahiki kusameheka kuanzia mwezi wa tatu kufuatia upeanaji kulingana na mapendekezo ya mshirika wa biashara wa ESO kwamba imefanya vyema katika vigezo mbalimbali. Hivi vigezo hujumuisha:

- Thibitisho kwamba fedha zilitumika vyema kwa matumizi yanayostaki
- Mikutano angalau miwili na msaidizi wa shughuli za utendakazi
- Maelezo ya ubora wa biashara kwamba imeinuka kulingana na modeli yake kutokana na msaada wa fedha hizi

*Tambua kwamba: Ikiwa biashara yako iko nje ya Jiji la Columbus lakini katika mizani ya Kaunti Franklin, haitahitimu kusamehewa.

## Maswala ya Kiufundi na Usaidizi Kusuluhisha

***Nitawasilishaje maombi ya programu za ruzuku pamoja na mshirika wangu wa ESO?***

Huduma za Hazina ya COVID-19 ya Columbus-Kaunti ya Franklin wa Kuinua na Kunusuru Biashara Ndogondogo zinapeanwa kupitia jukwaa la technolojia kwa ushirikiano na Submittable. Mbia wako wa ESO akikufikia na maombi atakupa kiungo cha jukwaa la submittable. Kisha itabidi uunde akaunti ya submittable bila malipo ili kuwasilisha fomu hizi kwa kujaza fomu ya **unda akaunti yako**. Utaulizwa ujaze jina lako, baruapepe na nywila ili kuunda akaunti. Akaunti ikishaundwa utaelekezwa kwa fomu ya uwasilishaji mahali unaweza kumwalika mbia wako wa ESO ashirikiane nawe kwa kubonyeza kiungo cha **Alika Wabia** katika sehemu ya juu upande wa kulia wa ukurasa. Wewe na mbia wako wa ESO mwaweza kushirikiana katika utayarishaji wa fomu hii ya kutuma maombi. Barua ya maombi ikishakamilika na kumaliziwa, utaweza kuwasilisha maombi kwa kubonyeza kitufe cha **Wasilisha** kilicho chini ya ukurasa.

***Nina maswala ya shida za kiufundi nikiwasilisha maombi yangu. Nitawasiliana na nani kwa usaidizi?***

Ikiwa una maswali yoyote na/ au umepata shida za kiufundi, tafadhali angalia utakavyosuluhisha swala hili kupitia kiungo hiki: SubmittableHelpCenter. Kwa maswali bayana ya kiufundi tafadhali wasiliana na timu ya msaada kwa mteja ya submittable katika support@submittable.com.